# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

**FAHARI YA SAME**

*Maendeleo Daima*

*Toleo la Septemba, 2023 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022*

## KANDA TATU ZA KIUCHUMI KUIINUA SAME.



***Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande akiangalia mazao katika bustani kwenye banda la maonesho ya nanenane la Same***

Katika jitihada za kuboresha kilimo na kuinua uchumi wa wakulima Halmashauri ya Wilaya ya Same imegawa Kanda tatu za Uchumi wa Kilimo ambazo wakulima watapewa elimu juu ya aina ya mazao ya chakula na biashara yanayoweza kustawi katika Kanda hizo.

Akizungumza katika maonesho ya Nanenane Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika katika viwanja vya Themi,Njiro mkoani Arusha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe. Yusto Mapande alisema kwa muda mrefu wakulima wilayani humo wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea ambacho hakijaweza kuwainua kiuchumi.

“Tumeamua kugawa Kanda tatu za kilimo ambazo ni Ukanda wa Tambarare ambao unalimwa Mkonge na mbogamboga katika eneo la umwagiliaji la Ruvu,Ukanda wa Kati ambao unalima Mpunga na Ukanda wa juu milimani ambao unalima Tangawizi na kwa sasa tunahimiza sana kilimo cha parachichi na tayari tumeshaanzisha vitalu vya miche ya parachichi” alisema Mapande

Amesema ili kufanikisha malengo ya kuinua uchumi wa wakulima Halmashauri inatengeneza miundombinu ya umwagiliaji ili kuwasaidia wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea cha kutegemea mvua za msimu.

“Sambamba na kuboresha miundombinu pia tunahakikisha wakulima wanapata pembejeo za kilimo kwa wakati ambapo tunatumia mawakala wa pembejeo waliopo katika maeneo yetu yote” amesema Mhe.Mapande.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba amesema maafisa Ugani wa Halmashauri waliopo katika Kata wamekuwa wakiendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya njia mbalimbali za kuboresha kilimo.

“Njia nyingine ya kutoa elimu kwa wakulima wetu ni kupitia maonesho haya ya Nanenane,hapa tumekuja na wakulima wetu ambapo pamoja nakutangaza bidhaa zao lakini wanajifunza mbinu mbalimbali za kilimo kutoka kwa wenzao wa maeneo mengine” amesema Bi.Tutuba.

Mkurugenzi huyo amesema kwa mwaka wa fedha ulioishia June 2023, Divisheni ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi ilitumia shilingi milioni 116 katika kuboresha kilimo na ufugaji wilayani humo.

Akizungumza katika Maonesho hayo, Mwenyekiti wa wakulima wa Tangawizi Kata ya Myamba Bw.Mbaraka Ally amesema "Faida kubwa ya kushiriki maonyesho ya nanenane ni kutangaza bidhaa yetu ya Tangawizi ambayo inatoka Mamba-Myamba, ambapo Tangawizi yetu ina ubora wa hali ya juu"

Bw.Eliniokoa Joseph ambaye ni Mkazi wa Arusha anasema" Nimekuja kwenye Banda la Maonesho la Same mahususi kwa ajili ya kununua Tangawizi ya Same, nimeshaitumia,ni nzuri sana na  inaponya mafua na magonjwa madogo madogo ni nzuri".

Maonesho ya Nane nane ya mwaka 2023 yamebebwa na kaulimbiu isemayo "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu wa Chakula"

## RAS AAGIZA HALMASHAURI KUWEKA KWENYE MFUKO MAALUM ASILIMIA 10 YA MAKUNDI MAALUM



*Katibu Twala Msaidizi Utawala wa Fedha na Ufuatiliaji Mkoa wa Kilimanjaro Bw. Posencian Kirumbi*

Halmashauri za Wilaya Mkoani Kilimanjaro zimeagizwa kuendelea kutenga na kuweka kwenye akaunti maalum fedha za uwezeshaji

wanawake,Vijana na watu wenye ulemavu zisubiri hadi serikali itakapotoa muongozo juu ya utaratibu wa ukopeshaji wa fedha hizo.

Agizo hilo limetolewa na Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Kilimanjaro anayesimamia Utawala wa Fedha na Ufuatiliaji Bw. Posencian Kirumbi wakati akizungumza katika kikao cha baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Same.

"Itakumbukwa kwamba Serikali ilisitisha utoaji mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kutafuta njia bora zaidi ya utoaji wa mikopo hiyo, hivyo fedha hizi ziendelee kutengwa kila robo hadi Serikali itakapotoa maelekezo"alisema Bw. Posencian.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba alisema kuwa Halmashauri hiyo imekuwa ikitenga fedha hizo na inaendelea kuzitenga na zimewekwa kwenye akaunti maalum.

Amesema katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Halmashauri imetoa mkopo wenye thamani ya **Tsh 186,006,300** kwa vikundi 75 Kati ya vikundi hivyo Vijana **18,** Wanawake **42** na Watu wenye ulemavu **15** aidha kiasi cha **Tshs 310,500,000.00** kimehamishiwa kwenye akaunti ya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu ikisubiria maelekzo ya Serikali.

"April 14 mwaka huu ndio serikali ilisitisha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 ya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na sisi tumeendelea kutenga fedha hizo na kuzihifadhi ili kusubiri maelekezo ya Serikali" alisema Bi. Anastazia.

Nae Diwani wa Viti Maalum Bombo Bi.Happiness Mchome ameiomba Serikali kutoa maelekezo mapema juu ya utaratibu wa utoaji wa fedha hizo kwa wanawake,vijana na watu wenye ulemavu kwani zilikuwa zinawasaidia kiuchumi.

## DC ATAHADHARISHA KUHUSU MVUA ZA ELNINO.

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amewataka wananchi wanaoishi maeneo hatarishi ambayo hupata athari za Mafuriko au maporomoko ya miamba (landslides) kuhama maeneo hayo kwa muda ili kupisha mvua za Elnino zinazotarajiwa kunyesha mwezi huu wa Oktoba 2023.

Agizo hilo la Mkuu wa Wilaya linakuja kufuatia taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuwa Wilaya ya Same iliyopo Mkoani Kilimanjaro ni Miongoni mwa Wilaya zilizotabiriwa kuwa na mvua kubwa za Elnino kuanzia mwezi Desemba 2023.

Amesema kutokana na Utabiri huo tayari Wilaya ya Same imeshaunda Kamati za Maafa za Wilaya (Kamati Elekezi na Kamati ya Wataalam)

Kamati za Kata na za Vijiji kwaajili ya kujiandaa kwa njia mbalimbali ili kukabiliana na athari zinazoweza kusababishwa na mvua hiyo ambapo kwasasa Kamati hizo zinaendelea kutoa elimu kwa Wananchi katika Maeneo mbalimbali.

Ameyataja maeneo ambayo yamekuwa yakiathiriwa na maporomoko ya miamba (landslides) wakati mvua zinapokuwa nyingi katika Wilaya ya Same nayo ni baadhi ya vijiji katika Kata za Myamba, Msindo, Kirangare, Mpinji, Chome na Vunta.

Maeneo ya tambarare ambayo huwa yanaathiriwa na mvua ni maeneo ya Kata za Same, Njoro, Makanya, Hedaru, Ruvu, Maore na Kihurio ambapo maeneo haya hupokea maji yanayotoka katika maeneo ya milimani na hivyo kusababisha mafuriko.

Mkuu wa Wilaya ameziagiza Kamati za maafa za Wilaya, Kata na Vijiji kuendelea kutoa elimu na kuwashauri wananchi kuhama kwa muda katika maeneo hatarishi ili kupisha Mvua zilizotabiriwa kunyesha mwezi Desemba mwaka huu.

Amezitaja hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa na Wilaya ili kupunguza athari za Mafuriko ni pamoja na kuzibua mitaro na kuchimba

njia za dharura za kupitisha maji katika maeneo yote hatarishi ili kuruhusu maji kupita kwa urahisi.

Katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko tayari Wilaya imeshaandaa dawa mbalimbali pamoja na kuainisha hospitali, vituo vya afya na zahanati ambazo zipo katika maeneo yanayoonekana kuwa salama zitakuwa zinatoa huduma kwa wahanga.

"Nawasihi Wananchi wa Wilaya ya Same kuendelea kufuatilia na kuzingatia taarifa za Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania (TMA) ili kuweza kuchukua hatua kabla madhara hayajatokea

Aidha Wananchi waepuke kukaa chini ya miti, kutembea sehemu hatarishi kama kwenye mikondo ya maji na umeme hasa wakati Mvua ikiwa inanyesha kwani ni hatari kwa maisha yao.

''Nitoe angalizo pia kwa wanaotumia vyombo vya Moto waepuke kabisa kupita sehemu ambapo maji ni mengi,waepuke kupita maeneno ambayo maji yamefunika madaraja''.

''Pia wakati wote wananchi wanapaswa kuwa na akiba ya chakula, fedha, maji, na vifaa vya huduma ya kwanza majumbani mwao kwa kipindi chote cha matarajio ya mvua kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa''.

''Kila mwananchi ahakikishe anakuwa na namba ya simu ya kiongozi wake katika eneo analoishi iwe ni wa Kijiji au Kata ili aweze kutoa taarifa kunapokuwa na tatizo''.

Kwa upande wake Afisa wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) Wilaya ya Same Bw.Yegelagi Kachwele alisema mvua za Elnino katika Wilaya ya Same zinatarajiwa kuanza mwezi Desemba mwaka huu hadi February mwaka ujao.

# HUDUMA YA UPASUAJI MKUBWA KUPATIKANA VITUO VYOTE VYA AFYA SAME




***Mwanamke wa kwanza kufanyiwa upasuaji kwenye Kituo cha Afya Hedaru ambaye alipata mtoto wa kike na kumpa jina la Samia kama shukrani kwa Rais Samia Suluhu kufanikisha upatikanaji wa huduma za upasuaji.***

Wilaya ya Same imedhamiria kuhakikisha kuwa huduma ya upasuaji mkubwa inapatikana katika vituo vyote vya Afya ifikapo Juni 2024 ili kusogeza huduma za upasuaji karibu na wananchi.

Akizungumzia mipango hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba amesema kwasasa jumla ya vituo vya Afya vinne tayari vinatoa huduma ya upasuaji tena kwa ufanisi mkubwa.

Amevitaja vituo ambavyo tayari vimeanza kutoa huduma hiyo ni Kituo cha Afya Hedaru, Ndungu, Shengena, Kisiwani pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Same.

"Sera ya Afya ni kuhakikisha kuwa vituo vyote vya Afya vinatoa huduma ya Upasuaji na kwa kuanzia tayari vituo vyetu vitano vinatoa huduma ya upasuaji na mipango ipo vizuri ya kuhakikisha kuwa vituo vyote

vinaweza kutoa huduma ya Upasuaji, tunamshukuru sana Mama Samia katika kufanikisha suala hili" amesema Bi.Anastazia.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same, Dk. Alex Alexander amesema vituo vya Afya ambavyo bado havijaanza kutoa huduma ya Upasuaji ni vile ambavyo vipo katika hatua za umaliziaji wa ujenzi wa majengo ya upasuaji.

Amesema vituo vya Afya Ruvu, Myamba na Mtii vipo katika hatua za umaliziaji wa majengo maalum ya upasuaji na yatakamilika mwaka huu wa fedha na yatakapokamilika huduma zitaanza kutolewa.

"Zahanati hizi tatu tayari fedha zake za ununuzi wa vifaa imeshatengwa kwenye Bajeti ya fedha ya mwaka 2023/2024 hivyo yakikamilika tu tutanunua vifaa na tumeshaomba kupatiwa wataalam kwaajili ya huduma za upasuaji katika vituo hivi" amesema Dk. Alex.

Amesema kuwa kwa upande wa vituo vya Afya vya Vunta na Makanya vinasubiri uboreshaji ili viweze kuanza kutoa huduma ya upasuaji ambapo kituo cha afya Vunta kimeshatengewe shilingi milioni 500 kwaajili ya uboreshaji.

Wilaya ya Same yenye wakazi 300,303 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 ina Jumla ya Hospitali 2, moja ikiwa ni ya Serikali na nyingine ya Taasisi ya dini, Vituo vya Afya 11 ambapo 9 ni vya Serikali na Zahanati 64 ambapo 48 ni za Serikali.

## MKURUGENZI AWAONYA WATENDAJI KATA KUTOTUMIA FEDHA MBICHI



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same akizungumza na Watendaji wakati wa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa TAUSI na FFARS, pembeni yake ni Mkuu wa Wilaya ya Same ,Mhe.Kasilda Mgeni*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba amewaonya Watendaji wa Kata na Vijiji kuacha kutumia fedha mbichi za Serikali kabla ya kuzipeleka benki.

Bi.Anastazia ametoa onyo hilo wakati akifungua mafunzo ya Matumizi ya Mfumo wa Ukusanyaji mapato wa TAUSI na Mfumo wa Matumizi (FFARS) kwa Watendaji wa Kata na Vijiji ambapo alisema hairuhusiwi kutumia fedha ya Serikali bila kuipitisha benki.

“Ni marufuku kutumia fedha yoyote ya Serikali bila kuipitisha benki hata kama ni michango ya wananchi ni lazima ikusanywe iwekwe kwenye akaunti ya Kijiji au Kata ndipo itolewe kwaajili ya matumizi” alisema Mkurugenzi.

Aidha Mkurugenzi huyo aliwataka watendaji kuhakikisha wanadhibiti mapato yote ya Serikali katika maeneo yao ili kuongeza makusanyo ya Halmashauri ambayo ndiyo yanayowezesha utekelezaji wa Miradi ya maendeleo.

Bi.Anastazia ameagiza Watendaji kuhakikisha kuwa magari yote yanayoingia Vijijini kupakia mazao kwaajili ya kusafirisha yawe yanakatiwa ushuru kwa kutumia Mfumo wa TAUSI na sio vinginevyo.

Akizungumza baada ya kushiriki mafunzo hayo Mtendaji wa Kata ya Hedaru Bw. Jackson Mbwambo alisema Mafunzo hayo yatawasaidia kusimamia vema ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Mfumo wa TAUSI.

"Tunaishukuru Halmashauri yetu ya Same kwa kutupatia Mafunzo haya ya kutumia Mfumo wa TAUSI, tunachoweza kumuahidi Mkurugenzi ni kwamba tutaongeza ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri yetu" alisema Mbwambo.

Jumla ya Watendaji wa Kata 34 na Watendaji Vijiji 100 wamepatiwa Mafunzo ya ukusanyaji mapato kwa kutumia Mfumo wa TAUSI na mafunzo ya Matumizi Serikalini kwa kutumia Mfumo wa FFARS.

## DC SAME AMUONYA MWEKEZAJI WA SHAMBA LA MKONGE.



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni akizungumza na Wananchi wa Kata ya Maore na Ndungu.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe. Kasilda Mgeni amemuonya mwekezaji wa shamba la Mkonge la LM Investment kuacha kutoa taarifa mitandaoni kwamba wananchi wamevamia na kuchoma moto eneo lake wakati sio kweli.

Mkuu wa Wilaya ametoa onyo hilo wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ndungu na Maore ambazo zinapakana na shamba hilo ambapo alisema taarifa za mwekezaji huo zinazorushwa mitandaoni zinazua taharuki.

"Nimetembelea eneo linalolalamikiwa na nimekagua maeneo yote ya shamba hilo yanayopakana na wananchi lakini eneo pekee nililokuta limechomwa na kusafishwa ni eneo panapojengwa shule ya Sekondari" alisema Mkuu huyo.

Mkuu wa Wilaya alimtaka Mwekezaji huyo kuacha kuzua taharuki mitandaoni kwani eneo lake lipo salama na hakuna mtu aliyevamia eneo hilo kwani eneo linalosafishwa ni mali ya Kijiji cha Misufini.

Mapema mwezi Agosti mwaka huu Serikali ilipunguza ekari 300 kutoka katika shamba la LM investment na kuzigawa kwa vijiji vya Mpirani, Misufini na Ndungu ambapo kila kijiji kilipata ekari 100.

Akizungumza katika Mkutano huo Diwani wa Kata ya Maore Bw.Issa Rashid alimueleza Mkuu wa Wilaya kuwa hakuna mwananchi yeyote aliyevamia eneo la mwekezaji.

"Huyu mwekezaji yupo hapa miaka mingi sana na hata kipindi kile tunahangaika tugaiwe maeneo kwaajili ya wananchi wetu tulikuwa wavumilivu zaidi ya miaka kumi hadi tukagaiwa eneo letu sasa leo tumeshapewa eneo ndo tuje tufany fujo" alihoji diwani huyo.

Diwani huyo alimuahidi Mkuu wa Wilaya kwamba Wananchi wake hawatafanya fujo yoyote wala hawawezi kuvamia eneo la Mwekezaji ila wanachosubiri wao ni kupatiwa hati miliki za maeneo waliyopewa.

# SAME YAOMBA KUONGEZEWA BAJETI YA MIRADI



*Zahanati ya Suji-Malindi*

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Same Bi.Hamisa Chacha ameiomba Serikali kuiongezea Wilaya ya Same kiasi cha fedha zinazokadiriwa kwaajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutokana na jiongrafia ya milima na miamba katika Wilaya hiyo ambayo inaongeza gharama ya ujenzi.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani katibu huyo amesema makadirio ya ujenzi yanayofanywa na Wizara wakati mwingine inaleta changamoto katika utekelezaji wa Miradi kwani fedha zinakuwa hazitoshi.

"Serikali inaleta fedha za kujenga darasa moja kwa shilingi milioni ishirini hadi ishirini na tano pamoja na kuweka madawati,fedha hii katika maeneo yetu ni ngumu sana kukamilisha darasa kutokana na jiografia ya huku" amesema Bi.Hamisa

Amesema katika sehemu nyingi ambazo Miradi inatekelezwa katika Wilaya ya Same wahusika wanalazimika kusafiri umbali usiopungua kilomita 70 kufuata vifaa vya ujenzi ambapo wakati mwingine hata garihaiwezi kufika katika eneo la ujenzi hivyo kulazimika kutumia vibarua kubeba na kuvifikisha site.

Bi.Hamisa amesema katika kusafirisha vifaa tuu tayari makisio ya bajeti yanaanza kuleta shida maana bajeti ilivyotengenezwa haikukadiria umbali wa kusafirisha vifaa wala haijakadiria gharama za kukata mlima na kusawazisha ili kupata eneo la ujenzi.

“Niiombe Serikali isitukadirie bajeti ya ujenzi wa darasa sawa na wakazi wa Kinondoni au maeneo mengine ya tambarare maana jiografia yetu ni ngumu na waje watembelee kujionea” amesema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba amesema gharama za ujenzi katika maeneo ya milimani ni kuwa na tayari wameshaomba Serikali kuwaongezea fedha ili Miradi iweze kukamilika.

“Tuliomba kuongezewa fedha za miradi kutokana na jiografia yetu na zimeongezwa lakini ndo tumeambiwa tulaze tofali na ukilaza tofali zinaenda nyingi hivyo kunakuwa hakuna nafuu, tunajazia fedha za mapato ya ndani ili Miradi ikamilike lakini Miradi ni mingi hatuwezi kuikamilisha yote kwa mapato ya ndani” amesema Anastazia.

## TANESCO HAKIKISHENI TAASISI ZOTE ZA SERIKALI ZINAPATA UMEME-MWENYEKITI.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande amelitaka Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) Wilaya ya Same kuhakikisha kuwa majengo yote ya Taasisi za Serikali yanapata huduma ya Umeme.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya TANESCO Wilaya ya Same iliyowasilishwa katika Kikao tangulizi cha Baraza la Madiwani (Pre-Baraza) Mwenyekiti huyo aliitaka TANESCO Wilayani humo kuweka Mipango ya kuhakikisha kuwa Taasisi zote za Serikali zinapata Umeme.

“Huduma ya umeme ni muhimu mjini na Vijijini,TANESCO jitahidini muhakikishe kuwa huduma ya umeme inafika katika majengo yote ya serikali,kwani inapofika katika majengo ya serikali hata vijiji vilivyo jirani vinanufaika” alisema Mhe. Yusto.

Kwa upande wake Meneja wa TANESCO Wilaya ya Same Mhandisi Fabian Ruhumbika alimwahidi Mwenyekiti kuyafanyia kazi maelekezo yake ya kufikisha umeme katika taasisi za serikali.

Alisema Shirika hilo limekuwa likitoa kipaumbele kwa taasisi za serikali kwa kadri bajeti inavyoruhusu ambapo alisema kwa kuona umuhimu wa kufikisha umeme katika taasisi za serikali tayari hospitali mpya ya Wilaya ilishapatiwa umeme tena kupitia maombi ya dharura.

“Shirika limekuwa likitoa kipaumbele kwa taasisi na miradi ya Serikali maana kuna maeneo hayakuwepo kwenye bajeti ya kupatiwa umeme kwa mwaka uliopita laki yaliweza kupatiwa kutokana na umuhimu wake ikiwemo hospitali ya Wilaya pamoja na Zahanati ya Saweni”alisema Mhandisi Ruhumbika.

Akitoa taarifa ya utekelezaji katika kikao hicho, Meneja huyo alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wameweza kusambaza umeme katika vijiji 11 ambavyo havikuwa na umeme kabisa.

Alisema kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2023 TANESCO Wilaya ya Same ilitumia Milioni 563.3 kutekeleza Miradi mbalimbali.

Kwa sasa taasisi za Serikali ambazo zinasubiri kupatiwa huduma ya umeme katika Wilaya ya Same ni pamoja na Kituo cha Afya Ruvu, Kituo

cha Afya Myamba na baadhi ya shule za Sekondari ikiwemo Moipo Sekondari  baadhi ya Ofisi za Kata na Vijiji.

## KANISA KATOLIKI SAME WATAMBULISHA ALIZETI MIBA ISIYOLIWA  NA TEMBO.



***Afisa Kilimo wa Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Bw. Berthold Msita akimweleza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bi.Anastazia Tutuba juu ya Alizeti Miba (Katam)***

Kanisa Katoliki Jimbo la Same linatekeleza Mradi Jumuishi wa Kilimo ambapo katika Mradi huo Kanisa kupitia kitengo cha kilimo limetambulisha mbegu ya Alizeti ambayo haiathiriwi na Tembo wala ndege.

Wilaya ya Same ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimepata madhara makubwa yatokanayo na Tembo ambapo kila mwaka zaidi ya ekari 2000 za mazao huathiriwa na Tembo kila mwaka hivyo mbegu hii inaweza kuwa suluhisho la tatizo la Tembo kuvamia mazao.

Akieleza faida za mbegu hiyo Afisa Kilimo wa Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Bw.Berthold Msita amesema mbegu hiyo inapoota majani yake yanakuwa yamezungukwa na miba na hivyo kufanya Tembo waiogope.

“Nashauri kwa wakazi wanaoishi maeneo yaliyozungukwa na Tembo wabadili aina ya mazao wanayolima na kuhamia kwenye kilimo cha Alizeti hii ambayo ni ya miba na ina uwezo wa kuzaa kwa wingi na kutoa mafuta mengi tofauti na mbegu ya alizeti zilizozoeleka” amesema Bw.Msita

Amesema tayari Kanisa hilo limegawa mbegu hiyo katika Kata ya Kisiwani na Mabilioni ambayo ni maeneo yanayoathiriwa sana na Tembo na zimeshaanza kuleta manufaa kwa wakulima.

Afisa Kilimo huyo pia alisema wametambulisha kwa wakulima mbegu ya maharage meupe ambayo yanasaidia katika kufukuza nyoka na wadudu ambao wanaleta uharibifu wa mazao shambani.

“Kuna mbegu ya maharage meupe ambayo inafukuza nyoka na wadudu wengine waharibifu wa mazao na mbegu hii kwa Same tumeigawa eneo la Mabilioni ambapo wakulima wameshaanza kuitumia na wanapoipanda hakuna haja ya kutumia tena dawa za viuadudu”amesema Bw.Msita.

## WAKULIMA SAME WASHAURIWA KUTUMIA VEMA MSIMU WA VULI

Wakulima katika Wilaya ya Same wameshauriwa kutumia vema msimu wa Mvua za Vuli kwani ndio msimu ambao umekuwa na mavuno makubwa kwa wakulima wilayani humo.

Wito huo umetolewa na Mratibu wa Maonesho ya nane nane 2023 kutoka Wilaya ya Same, Bi. Yulia Joel ambaye alisema msimu wa mvua za vuli ndo msimu mkubwa wa kilimo na wenye mavuno mazuri katika Wilaya ya Same.

" Kwetu msimu wa vuli ndio msimu mkubwa hivyo wakulima wautumie vema wakizingatia pia ushauri wa kitaalam ikiwemo aina ya mbegu za

kutumia,viua dudu na mbolea ambazo zitaleta tija katika mazao”
alishauri Bi.Yulia

Aidha Mratibu huyo ametoa ushauri wa aina ya mbegu za mahindi na maeneo zinakoweza kutoa mavuno mengi katika eneo dogo kuwa ni (SEED CO 403) ambayo inastawi vizuri katika ukanda wa chini, (SEED CO 419) ambayo inastawi ukanda wa kati, (DK 8031) ambayo inastawi ukanda wa chini (ukanda ambao una mvua ndogo) pia kuna( DK 80 30 89) ambayo inastawi ukanda wa juu. " Hivyo tunafanya maonyesho ya kuonyesha kwamba haya mazao yote tuliyonayo yanafanya vzuri kwenye maeneo yetu ya Same ," alisema Bi Yulia.

Bi Yulia ameshauri pia wakulima kufuata kanuni bora za kilimo na kupata ushauri wa mara kwa mara kwa maafisa kilimo walio katika maeneo pamoja na kupanda kwa wakati, kupalilia kwa wakati pia kutumia mbegu bora kwasababu chanzo kikubwa cha uzalishaji kwa wingi ni mbegu bora na mbolea.

Pia, anaeleza kuwa kutokana na udongo kutumika kwa muda mrefu umepoteza virutubisho vyake,hivyo ni vizuri kwa wakulima kutumia mbolea bora ili kuzalisha kwa tija ambapo alisema kwa kilimo cha mahindi iwapo mtu atazingatia kanuni bora za kilimo anaweza kuvuna hadi gunia 30 kwa ekari.

Katika maonesho hayo, Bw.Paulo Mtango, Mkulima Kiongozi kutoka Gonja,wilayani Same amekuja na ubunifu wa kutengeneza mbolea,viuadudu na booster za mazao za asili ambazo zinasaidia katika kupunguza gharama za kilimo.

# CCM YAWATAKA WANANCHI KUSHIRIKI MSARAGAMBO



*Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Same Comred Abdallah Mnyambo (kulia) akiwa katika ziara kwenye shule ya Sekondari Kimala, Kata ya Mpinji.*

Wananchi Wilayani Same wametakiwa kuchangia nguvu kazi katika Miradi mbalimbali ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali katika Maeneno yao.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Same Comred Abdullah Mnyambo wakati akizungumza na Wananchi wa Kata ya Mpinji alipokuwa katika Ziara ya kukagua Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025.

Comred Mnyambo amesema kuwa SErikali inapoleta fedha kwaajili ya Utekelezaji wa Miradi inatambua kuwa kuna michango (nguvukazi ) za wananchi ambazo zitatumika ili fedha zilizoletwa ziweze kukamilisha Mradi husika.

Katika Kata ya Mpinji Mwenyekiti huyo akiwa amefuatana na Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Same alitembelea shule ya Sekondari Kimala ambayo inajengwa Bweni la Wanafunzi wa Kidato cha tano na sita.

“Fedha zilizopokelewa hapa kwaajili ya Ujenzi wa Bweni hadi kuweka vitanda ni shilingi Mil.260 ambazo kimsingi hazitatosha bila wananchi kuchangia nguvu zao kwa kusawazisha eneo la ujenzi na hata kuchimba msingi” amesema Mwenyekiti huyo.

Mwenyekiti huyo aliwataka Viongozi wa CCM ngazi za Vijiji na Kata kuwa mstari wa mbele kujitokeza kushiriki shughuli za kijamii na kuwahamasisha wananchi wanaowaongoza pia kushiriki kuchangia nguvu zao katika Miradi ya Maendeleo.

Akizungumzia Ushiriki wa Wananchi Diwani wa Kata ya Mpinji Bi.Namkunda Izungo amesema wananchi katika eneo lake wamekuwa wakishiriki kikamilifu kujitolea nguvukazi katika Miradi ya Maendeleo.

“Kwenye Kata hii wananchi wanashiriki sana katika Miradi tunayoletewa lakini wakati mwingine kazi zinachelewa kutokana na mazingira yetu ya milima ambapo kusawazisha eneo kunachukua muda mrefu” amesema Diwani huyo.

Akizungumzia Ujenzi huo Mwalimu wa Ujenzi katika Shule ya Sekondari Kimala Bw.Samson Ruhagi amesema Ujenzi unaendelea vizuri kwani upo katika hatua za umaliziaji na utengenezaji wa vitanda unaendelea.

Mwaka huu shule hiyo imepokea jumla ya Wanafunzi 208 wa kidato cha tano kati ya  Wanafunzi 283 waliopangiwa shuleni hapo.



*Bweni la wanafunzi shule ya Sekondari Kimala*

## MNADA WA MIFUGO WAZINDULIWA KIRINJIKO.



Halmashauri ya Wilaya ya Same, Mkoani Kilimanjaro imezindua mnada na soko la barabarani katika eneo la Kirinjiko kwa lengo la kuongeza mapato na kuwawezesha wananchi watakaofika katika Hospitali mpya ya Wilaya iliyo jirani na eneo hilo pamoja na wasafiri kupata huduma katika mnada huo.

Mnada huo ulizinduliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo Bi.Kasilda Mgeni Mapema mwezi Septemba mwaka huu ambapo aliwahimiza wananchi wa Same kutumia vema fursa hiyo katika kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza katika Uzinduzi huo kuu wa Wilaya ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Soko ambao umekamilika kwa awamu ya kwanza .

“Ndugu zangu wafugaji wa Wilaya hii ya Same na Wilaya za jirani niseme tuu kwamba Mnada huu ni wa kwenu, Serikali imewajali kwa kuwajengea mnada huu, hivyo muutumie vizuri na kutunza miundombinu iliyopo” alisema Mkuu huyo.

Hata hivyo Mkuu wa Wilaya ya Same alisema kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022 inaonyesha Wilaya ya Same ina jumla ya Ng’ombe laki moja

na tatu, Mbuzi laki moja na kumi na saba elfu kondoo sabini na tatu elfu na sita themanini na nne.

“Tumeanzisha mnada huu kama fursa ya kiuchumi kwa wafugaji na wananchi wengine wa Same lakini pia mnada huu pamoja na soko la barabarani ni huduma kwa wananchi wa Same na hata wasafiri wanaotumia barabara ya Same-Dar es Salaam” alisema Mhe.Kasilda

Hata hivyo Mkuu wa Wilaya aliwataka wafugaji kuwa na utaratibu wa kupunguza mifugo kwa kuiuza wakati wa kiangazi ambapo malisho ni haba na kununua mingine pale kiangazi kinapokwisha ili kuepuka hasara ya mifugo kufa kwa kukosa malisho.

Akizungumza katika Uzinduzi huo Mkurugenzi wa Wilaya ya Same Bi. Anastazia Tutuba alisema Wilaya imejitahidi kuhakikisha kwamba huduma zote muhimu zinapatikana katika eneo hilo ili kuwawezesha wafanyabiashara kutumia vema eneo hilo.

“Hapa kuna huduma ya Umeme, maji, vyoo na hata barabara za eneo hili ni za uhakika na tayari tumeshagawa maeneo zaidi ya 500 ya kujenga vibanda vya biashara na kuchomea nyama”alisema Mkurugenzi huyo.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Same Mhe. Yusto Mapande alisema lengo kuu la Serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanajikwamua kiuchumi hivyo soko hilo litasaidia kukuza uchumi wa Wananchi.

“Jambo ambalo wananchi wanalitarajia kutoka kwa viongozi wao ni kuwaonyesha njia ambayo itatatua matatizo yao ikiwa kuwaletea fursa ya ajira na fursa za kiuchumi na katika eneo hili hadi sasa kuna ajira zaidi ya mia sita”alisema Mapande



*Madiwani wapya Mheshimiwa Jofrey Jofrey(kushoto) wa Kata ya Kalemawe na Mheshimiwa Omar Abdallah (kulia) wa Kata ya Njoro wakifuatilia kikao chao cha kwanza cha Baraza la Madiwani mara baada ya kuapishwa.*



*Wakuu wa Idara za Halmashauri ya Wilaya ya Same wakifuatilia kikao cha Mwaka cha Baraza la Madiwani kutoka kushoto ni Maurie Kambangwa (Mhandisi Ujenzi),Elisha Kapama (Afisa Mipango Msaidizi) na Ally Mngwaya (Afisa Misitu).*


***Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same wakiwa katika picha ya pamoja na Madiwani wapya wa Kata za Njoro na Kalemawe kama ishara ya kuwakaribisha katika Baraza la Madiwani.***



***Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Same Wakiwa katika ziara ya kufuatilia Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025).Hapa Wakiwa katika Kata ya Mpinji kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya,Ndg.Abdillah Mnyambo,Diwani wa Kata ya Mpinji Ndg.Napenda Izungo na Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Yusto Mapande.***



**JARIDA MTANDAO WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138,SAME**

***Mhariri wa Mkuu:Anastazia Tutuba***

***Mhariri wa Habari:Amina Sangawe***

***Toleo la Septemba, 2023 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***